AN **ENGAGE** PRESENTATION

# KUJUMUISHA IDADI YA WATU, AFYA NA MAZINGIRA

## KWA MAENDELEO YANAYOTEKELEZWA KENYA

## MWONGOZO WA UWASILISHAJI



USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

# Mwongozo wa Uwasilishaji

## KUJUMUISHA IDADI YA WATU, AFYA NA MAZINGIRA KWA MAENDELEO YANAYOTEKELEZWA KENYA


### SHUKRANI

"Ujumuishaji wa idadi ya watu, afya na mazingira katika maendeleo endelevu nchini kenya" ni chombo cha utetezi cha mawasiliano ambacho kilipangwa na PHE Kenya Multimedia Taskforce inayoongozwa na National Council for Population and Development kwa ushirikiano na Population Reference Bureau.

Shukrani ya kipekee kwa PHE ENGAGE Taskforce ya Njia Nyingi kwa Aliyotoa ya muhimu kwa "kujumuisha Idadi ya watu, Afya na Mazingira kwa Maendeleo Yanayotekelezwa Kenya."

Uwasilishaji huu wa Midia-Anui umetengenezwa kwa ufadhili wa shirika la United States Agency for International Development (USAID) kulingana na makubaliano ya ushirikiano AID-OAAA-A-16-0002. Habari inayotela ni jukumu la NCPD na PRB na sio serikali rasmi ya Marekani na hivyo basi,mazulio yanayotolewa hayaonyeshi au kunukuu mawazo au maono ya shirika la USAID ama Serikali ya Marekani.



© 2017 Population Reference Bureau. Haki zote zimehifadhiwa.


## YALIYOMO


IUTANGULIZI WA MWONGOZO WA UWASILISHAJI ............ 1

MADHUMUNI YA WASILISHAJI ............................... 1

NAFASI ZA UWASILISHAJI .................................... 1

UWASILISHAJI WA WASIKILIZAJI MBALIMBALI ............... 2

MASWALA YA ZIADA.......................................... 2

UWASILISHAJI WA USISHO-JUMLISHI ........................ 3

UJUMBE MAALUM KUTOKA KWA MAANDISHI ...............16

MWONGOZO WA MJADALA ................................ 21

MASWALA YANAYOULIZWA MARA KWA MARA ............. 23

NYENZO ZAIDI ............................................ 26


NCPD

PACE Policy Advocacy Communication Enhanced

PRB INFORM EMPOWER ADVANCE

## Utangulizi Wa Mwongozo wa Uwasilishaji

TMwongozo huu wa uwasilishaji umeundwa ili kusaidia wateja waweze kunufaika kwa kiwango cha juu kutokana na uwasilishaji wa “Kujumuisha Idadi ya Watu, Afya na Mazingira Kwa Maendeleo Yanayotekelezwa Kenya” ENGAGE pamoja na uwasilishaji wa mwongozo wa PRB ENGAGE. Mwongozo wa Uwasilishaji umejumuisha maswala ya nyongesa yasiyo ya kifani kama vile makala kamilifu ya uwasilishaji, marejeleo, jumbe mahususi zikiandamana na picha; FAQS; na mwongozo wa majadiliano unaoweza tumika kuwezesha mwingiliano na mazungumzo baina ya watazamaji.

Baada ya kukagua mwongozo huu wa uwasilishaji utaweza kutambua jinsi ya:

- Kukagua mbinu za kutumia uwasilishaji wa ENGAGE kwa kaumu mbali mbali.
- Kujibu maswali yanayoulizwa mara kwa mara juu ya uwasilishaji huu.
- Kuzua mazungumzo na wasikilizaji juu ya ujumbe mahususi katika uwasilishaji huu.

## Madhumuni ya Wasilishaji

Lengo la uwasilishaji mseto wa “Kujumuisha Idadi ya Watu, Afya na Mazingira Kwa Maendeleo Yanayotekelezwa Kenya” ENGAGE, ni kujenga mwamko na kuongeza usaidizi kwa muelekeo wa idadi jumuishi, afya na mazingira (PHE) nchini Kenya.

Ili kuweza kufikia lengo hili, uwasilishaji huu umeundwa kwa njia ya kuinua uelewa wa yeyote jinsi ya PHE inashughulikia maswala tata na yenye mwingiliano katika maswala ya upangaji uzazi, kupata huduma za kiafya, ustawishaji wa maliasili na mbinu za uchumaji riziki zinazozikumba familia zinazoishi mashambani na jumuia katika nchi zinakua.

Kaumu ya wanaolengwa na mswada inajumuisha washika-dau wa sera katika serikali; wafadhili wanaojishughulisha na maswala ya Uzazi; jinsia na maswala ya mazingira; viongozi katika sekta ya afya na mazingita; maafisa wa mipango; wanahabari na wengine.

Malengo maalumu ya uwasilishaji huu ni:

- Kueleza jinsi mbinu ya PHE inafanya kazi kustawisha afya, makaazi, ulinzi wa chakula na mali asili.
- Eleza ufanisi wa mswada kadhaa ya PHE nchini Kenya.
- Jenga mazungumzo baina ya wasikilizaji washiriki juu ya nia ya wekezaji kwa miswada mseto ya PHE.

## Nafasi za Uwasilishaji

Uwasilishaji huu wa ENGAGE wa vifaa vya matumizi ni wa wataalamu wanahusika katika viwango vyote vya upangaji uzazi, afya, na mazingira iwe katika akademia, mswada na mazingira ya kijamii. Wanaokusudiwa na uwasilishaji huu ni:

- Msingi: Waundaji wa seraa wa serikali katika viwango vyote na wafadhili wa maendeleo walio na uwezo wa kugawa rasilimali na kuendeleza PHE kimswada na kimpango nchini Kenya.
- Sekondari: Wale wote wanaowashawishi waundaji miswada wa kiwango cha juu-waandishi wa habari, raia, viongozi wa kidini, maofisa wa mipango na viongozi wengine katika jamii.

## Uwasilishaji wa Wasikilizaji Mbalimbali

Uwasilishaji huu wa ENGAGE, umeundwa kutumika kwa mandhari au mazingira kadhaa, hasa wakati Kenya inapotekeleza malengo ya maendeleo endelevu, na kulenga mengineyo. Baadhi ya njia ambazo uwasilishaji huu unaweza kutumika kufikia watu mbalimbali ni kama zifuatazo:

### WAUNDAJI MISWADA

- Wajuvye waundaji miswada juu ya umuhimu wa kuwekeza na PHE nchini Kenya.
- Onyesha ufanisi na utekelezaji faavu wa mtazamo wa PHE nchini kenya na kwingineko.

### WATETESI WA UPANGAJI UZAZI

- Waelemishe watetesi hawa juu ya kusisitiza uhusiano wa upangaji uzazi, afya na mazingira.
- Ongea na wale wanaohudhuria vikao vya afya ya jamii au mikutano ya washikadau wenye ujuzi wa mtazamo ya PHE.
- Elezea vile mtazamo wa PHE unavyofanya kazi kwa wanaume na wanawake kwa jumla ili kustawisha maisha na kukinga maliasili.

### VIONGOZI VYA KIJAMII NA KIDINI

- Waelimishe viongozi wa kijamii na kidini juu ya manufaa yanayoletwa na mtazamo wa PHE kwa familia na jamii.
- Dumisha mazungumzo ya mswada na viongozi wa mashinani, wakiwepo wa kijamii na kidini katika mikutano ya semina na matukio mbalimbali.

### VYOMBO VYA HABARI

- Waelimishe wanahabari juu ya ufanisi wa mtazamo wa PHE, kwa kutumia uwasilishaji wa ENGAGE kama kifaa cha kufunzia.
- Tafuta nafasi ya mazungumzo katika runinga na redio, yanayohusisha kwa kiwango majadiliano na maswala juu ya PHE.

## Maswala ya Ziada

Unaweza kufanya uwasilishi huu uwe wa kuvutia zaidi kwa wasikilizaji wako kwa kuongeza ujumbe kuhusu matukio ya jumla na mazoezi katika maeneno mbalimbali nchini Kenya, hasa yale yanayoafikiana na wasikilizaji wako. Mambo ya kuzingatia unapokagua wasikilizaji wako ni kama:

- **Kiasi cha hadhira.** Unapokuwa na kikundi kidogo,unaweza kutoa uchanganuzi wa kina unaolingana na visa vya ukweli katika maisha au matukio kwa sababu unawajua washiriki wako katika kikundi. Kwa vikundi vikubwa huenda ukachukua muda mwingi wakati wa kuwasilisha waliyoandikwa ili kueleza dhana maalum na kuhakikisha ya kwamba uwasilisaji unamfaa kila unayetazama.
- **Kiwango cha uelewaji.** Ni vizuri kila mara kuchukulia ya kwamba hadhira haina uelewa wa istilahi za kiufundi ambazo unaweza kuzitumia katika uwasilishaji wako. Ikiwa unapeana uwasilishaji wa moja kwa moja,tunashauri ufuate maandishi na kutoa maelezo kwa istilahi ambazo zinaweza kuwa geni kwa baadhi ya washiriki.

# **UWASILISHAJI** WA USISHO-JUMLISHI

## Kujumuisha Idadi ya Watu, Afya na Mazingira kwa Maendeleo Yanayotekelezwa Kenya

### Toleo la ENGAGE

**Telezi/Slaidi 1**

*Kichwa Chake - Kujumuisha Idadi ya Watu, Afya Na Mazingira kwa Maendeleo Yanayotekelezwa Kenya*

Uwasilishaji wa Usisho-jumlishi

→ **Bonyeza Mbele 2**

Kenya ni kiongozi Afrika katika sera na mipango ya maendeleo…

→ **Bonyeza Mbele 3**

…yanayoendeleza ustawi wa kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa watu wake na inayoimarisha uchumi wake.[1,2,3]

→ **Bonyeza Mbele 4**

Kenya pia ilizindua Mikakati Ya Kitaifa Ya Kuimarisha Mabadiliko Ya Hali Ya Anga kuimarisha uthabiti na uwezo wana nchi kujirekebisha kutokana na mazingira yanayobadilika kwa haraka.[4]

→ **Bonyeza Mbele 5**

Mabingwa wa mazingira, kama marehemu Wangari Maathai, wanatufungua macho kuelewa umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

Sera hizi hudumisha afya…

→ **Bonyeza Mbele 6**

…na kuelekeza Kenya katika njia ya ukuzaji wa kiuchumi na maendeleo.

Hata hivyo, kinachohitajika kufanywa ni mengi...

→ **Bonyeza Mbele 7**

Ili kushughulikia yanayofanya idadi ya watu inayoongezeka haraka…

→ **Bonyeza Mbele 8**

…afya yetu na ustawi wetu…

→ **Bonyeza Mbele 9**

…na vile vile tunavyotumia mali yetu ya asili.

→ **Bonyeza Mbele 10**

Kenya inaweza kuongoza katika afya iliyoboreshwa, utekelezaji wa mazingira na maendeleo zaidi ya kiuchumi shugulikia changamoto zote tatu pamoja.

→ **Bonyeza Mbele 11**

Huu mtazamo wa Idadi ya Watu, Afya na Mazingira au PHE unatambua uhusiano tata kati ya watu, afya yao na mali ya asili wanayotegemea.

→ **Bonyeza Mbele 12**

PHE yashughulikia nguvu za idadi kupitia kwa upangaji uzazi wa hiari unaoimarisha…

→ **Bonyeza Mbele 13**

matokeo ya kiafya ya watu na watoto wao, na…

→ **Bonyeza Mbele 14**

vile vile watu wanahusiana na mazingira yao.

→ **Bonyeza Mbele 15**

PHE inajumuisha kutoa taarifa na huduma za upangaji uzazi kwa hiari na utunzaji wa afya ya kimsingi na utunzaji wa mali ya asili inayotekelezwa.

→ **Bonyeza Mbele 16**

Ebu ifikirie familia iliyomo Mashinani Kenya.

→ **Bonyeza Mbele 17**

Si rahisi kwao kufikia kliniki kila mara kwa sababu mara nyingi huwa mbali sana

→ **Bonyeza Mbele 18**

…lakini wahudumu hutoa huduma maluum za kimsingi na ya uzazi nyumbani mwao. Kutokana na haya, wazazi wanaweza kupanga na kuweka nafasi kati ya uzazi wa watoto wao na familia nzima huweza kupata huduma ya afya ya kimsingi.

→ **Bonyeza Mbele 19**

Familia huyategemea mazingira Kwa mahitaji yao ya kila siku: Kilimo huwapatia riziki na chakula,

→ **Bonyeza Mbele 20**

…msitu huwapa kuni ya kupikia

→ **Bonyeza Mbele 21**

…mifugo hupata malisho

→ **Bonyeza Mbele 22**

…ziwa hupeana maji safi ya kupikia na kufulia nguo.

Lisha Mazingire hutemewa, haana matumaini katika mali hizi kwani…

→ **Bonyeza Mbele 23**

…wanaweza kuzalisha mapato kutoka kwa kazi tofauti kama kazi ya mikono; wako na stovu inayohifadhi moto na kupikia vyakula vyao; na wanatumia kilimo, uvuvi, na njia za malisho.

Mienendo na maendelezo ya afya hukuza uthabiti wa familia…

→ **Bonyeza Mbele 24**

…dhidi ya dhiki za kimazingira zinazoharibu na kupunguza mali ya kiasili.

→ **Bonyeza Mbele 25**

Uthabiti wa familia huchangia afya bora, ongezeko wa usalama wa chakula na mapato zaidi ya kuwekeza kwa elimu na mahitaji mengine ya kinyumba.

→ **Bonyeza Mbele 26**

Mienendo hii ya kuendeleza ina athari kuu katika kiwango cha kijamii.

Haya yote yanajumuishwa na yanaweza kutolewa kama sehemu ya suluhisho changanuzi kwa maendeleo yanayodumishwa.

→ **Bonyeza Mbele 27**

Katika jamii ya mashinani – ambapo robo tatu (3/4) ya Wakenya huishi na ambapo miradi mingi changanuzi ya PHE ilipo – afya na riziki zimejumuishwa na mali ya asili au usalama wa chakula.[5,6]

→ **Bonyeza Mbele 28**

Lakini ongezeko la idadi ya watu haraka, matumizi ya mali yasiyodumishwa na mabadiliko ya hali ya anga yanaweza kuiathiri vibaya afya ya binadamu na yaweza kuathiri maisha ya mtu na maendeleo ya kiuchumi.

→ **Bonyeza Mbele 29**

Mazingira huathiri afya na ustawi wa watu na hata pale familia wanapoishi.

→ **Bonyeza Mbele 30**

Afya hafifu na muundo msingi wa usafiri – sana sana katika sehemu zilizo mbali na zizofikiwa kwa urahisi – huizuilia familia kupata huduma za kiafya.

→ **Bonyeza Mbele 31**

Uwezo wa kufikia palipo na huduma za afya ni muhimu kwa kuendeleza matibabu na ukigaji wa UKIMWI na malaria, maji na usafi na afya ya mama na mtoto.

→ **Bonyeza Mbele 32**

Huduma za afya za uzazi, hata upangaji uzazi, uathiri afya na ustawi wa familia na pia idadi ya ongezeko la watu.

Kwa mfano, katika jamii za sizojiweza za Kenya…

→ **Bonyeza Mbele 33**

…wanawake mara nyingi huwa na watoto wawili zaidi ya walivyotarajia. Kutokana na ayo, familia inahitaji rasilmali zaidi ili kumtosheleza kila mmoja wao ambayo huongeza umaskini kinyumbani na kitaifa.[7]

→ **Bonyeza Mbele 34**

Familia ikiwa na watoto wengi kuliko walivyotarajia, ongezeko la watu pia hukuzwa kwa haraka. Kwa chini ya miaka 30, idadi ya watu Kenya iliongezeka maradufu kutoka milioni 21 mwaka wa 1989 hadi milioni 44 mwaka wa 2015…

→ **Bonyeza Mbele 35**

…na inaelekea kufika watu milioni 64 ikifikia mwaka wa 2030.[8,9]

→ **Bonyeza Mbele 36**

Ongezo la haraka namna hii inaweza kuathiri mazingira.

→ **Bonyeza Mbele 37**

…na kuathiri vile watu wanavyotumia mali yao ya asili.

→ **Bonyeza Mbele 38**

Kilimo,

→ **Bonyeza Mbele 39**

misitu, na

→ **Bonyeza Mbele 40**

sekta ya uvuvi

→ **Bonyeza Mbele 41**

inawaajiri 75% ya wafanyikazi wa Kenya. [10,11]

→ **Bonyeza Mbele 42**

Ilichangia thuluthi ya GDP ya Kenya Jumla ya Pato la Kinyumbani katika mwaka wa 2016 na ni kiini katika mikakati yetu ya maendeleo.[12]

→ **Bonyeza Mbele 43**

Hadi sasa, mashamba yanaendelea kuwa madogo wakati wakulima wanawagawia wanao.

→ **Bonyeza Mbele 44**

Kwa hakika, thuluthi mbili ya wakulima Mashinani wanaamini…

→ **Bonyeza Mbele 45**

…kuwa mashamba yao hayawatoshi wanao kuendelea kuyalima.13

→ **Bonyeza Mbele 46**

Misitu inakatwa kwa kiasi kikubwa ili kupata nafasi ya kulima, malisho, kuni na kujenga majumba.[14]

→ **Bonyeza Mbele 47**

Maziwa yanapungua kwa samaki wanaovuliwa kwa mitindo ya uvuvi isiyodumu na matumizi ya viwanda.[15,16,17,18]

→ **Bonyeza Mbele 48**

Kwa kuongezea, mabadiliko na mitindo ya hali ya anga na matokeo ya kupita kiasi ya anga kama ukame huharibu mimea na mifugo…

→ **Bonyeza Mbele 49**

…inayoleta dhiki ya chakula…

→ **Bonyeza Mbele 50**

…uhaba wa mapato kwa familia…

→ **Bonyeza Mbele 51**

…na ongezeko la umaskini…

→ **Bonyeza Mbele 52**

…sanasana katika malishoni ya sehemu kame na kavu Kenya, ambayo ni asilimia 80 ya nchi na ni muhimu katika ya wafugaji.[19,20]

→ **Bonyeza Mbele 53**

Kwa hakika, mabadiliko ya anga inaathiri uchumi ambapo sekta nyingi zinapoteza pesa zinazokadiriwa kama dola bilioni 1 hadi bilioni 3 au bilioni 100 hadi 300 za shilingi za Kenya kila mwaka hadi kufikia 2030.[21]

→ **Bonyeza Mbele 54**

Wanawake na wasichana wanaathiriwa sana na mabadiliko ya anga.[22,23,24]

→ **Bonyeza Mbele 55**

Majukumu yao ya kinyumbani kama kutafuta kuni na maji na kilimo huwa mzigo mzito kwa sababu lazima watembee masafa marefu kutafuta kuni na maji na wajitahidi zaidi kukuza mimea katika mchanga ulioisha rutuba.

→ **Bonyeza Mbele 56**

Kwa kuongezea, kuna hatari zaidi ya mizozo ya watu na wanyama poli ambapo jamii nyingi zinahamia palipo na rasilmali nyingi ambapo huwa mkabala na palipoifadhiwa wanyama. Hapa, wanyama huweza kuharibu mimea au makazi.[25]

→ **Bonyeza Mbele 57**

Mali inayodididimia na njia finyu za kiuchumi za kuchumia mapato Mashinani zinawapa vijana wanaotaka na kuhitaji kupata riziki changamoto…[26]

→ **Bonyeza Mbele 58**

…na huwasukuma watu binafsi na familia kukimbilia jijini kutafuta ajira.

→ **Bonyeza Mbele 59**

Ongezeko la haraka ya makazi yasiyo na mpango linaleta changamoto kwa maafisa wa mji wanapojaribu kuyatimiza mahitaji ya kimsingi ya jamii.

→ **Bonyeza Mbele 60**

Mielekeo changanuzi katika maendeleo kama PHE inaweza kushughulikia kikamilifu changamoto kama idadi ya watu, afya, riziki na rasilmali kwa njia kamilifu inayozingatia mahitaji tofauti ya kijamii na kushughulikia changanuzi nyingi.

→ **Bonyeza Mbele 61**

Mielekeo ya PHE inakuza afya na ustawi wa wanawake, wapendwa na watoto wao kwa kufanya huduma za afya kupatikana kwa urahisi. Mielekeo ya PHE inakuza uwezo wa jamii tofauti kuendeleza matumizi ya rasilmali ya kimazingira na mitindo ambayo inakuza uthabiti wao katika mabadiliko ya anga na mabadiliko kwa ujumla.

Tuchunguze kwa undani vile mwelekeo wa PHE umekuza afya na ustawi wa familia nyingi, imewawezesha jamii nyingi na kusaidia kuhifadhi mali ya asili hapa Kenya.

→ **Bonyeza Mbele 62**

Afya ya Watu ya Mazingira – Mradi wa Kilindi cha Ziwa Viktoria au HoPE – LVB, ulianza kufanya kazi Kenya mwaka wa 2012. HoPE – LVB iliongeza upatikanaji wa huduma za afya na hata upangaji wa uzazi wa hiari. Kupitia mradi huu, waliooana wanaahirisha uzazi na kupata huduma za afya muhimu mpaka huduma za afya za mama na mtoto na huduma za ukigaji na matibabu ya UKIMWI na malaria. [27,28]

→ **Bonyeza Mbele 63**

Caren ambaye ni mwanachama wa kikundi cha kijamii cha wanawake anaeleza vile mradi huu umeiathiri familia yake:

→ **Bonyeza Mbele 64**

[MAHOJIANO: Caren Odek, mwanachama wa kijamii HoPE-LVB]

“Nilikuwa nafikiria kuwa kuwazaa watoto wengi kungemfanya mume wangu kunipenda zaidi. Kile ambacho sikukijua ni kwamba hayo ndiyo yangekuwa mwanzo shida…”

“Watoto wangu wangegonjeka kila mara na kwa kupata matibabu kulikuwa mbali sana…”

“Makazi yetu yalikuwa machafu bali hatukujali kwani hatukuwa na ujuzi wa umuhimu wa usafi wa mazingira…”

“Lakini baada ya mradi huu kuletwa, sasa tunaelewa vile tunatupa uchafu wetu ifaavyo…”

→ **Bonyeza Mbele 65**

Vile HoPE-LVB ilivyoongeza ujuzi na uasiliaji wa ujumbe wa huduma za afya za kimsingi, pia ilishughulikia mahhitaji ya usimamizi na mali ya asili na mazingira za jamii zinazohusiana. [29,30]

→ **Bonyeza Mbele 66**

Mradi huu ulishughulikia riziki na lishe yanayohusiana na mazingira katika jamii ya wavuvi. Uvuvi wa kupita kiasi na matumizi yasiyodumu ya ardhi yalididimisha idadi ya samaki na kuharibu ardhi iliyotegemewa na jamii.[31,32]

→ **Bonyeza Mbele 67**

Kutokana na haya, huu mradi uliwawezesha jamii katika mitindo ya kilimo inaayodumu ambayo imepunguza utegemeaji wa rasilmali moja na ikatoa asili mbalimbali za mapato na chakula.[33,34]

→ **Bonyeza Mbele 68**

Sarah, mwanamke atokaye sehemu ya mradi wa HoPE-LVB, anaelezea:

→ **MBonyeza Mbele 69**

[MAHOJIANO: Sarah Achieng' Onyango, mwanachama wa jamii ya HoPE-LVB]

"Nishajifunza vile naweza kuchanganya mimea ili nipate mazao ya ana tofauti…"

"Nina uhakika wa kupata chakula cha mwaka mzima. Mtazamo wangu kuhusu upandaji wa miti umebadilika na nishapanda miti ya aina tofauti…"

→ **Bonyeza Mbele 70**

Kujifunza ujuzi wa kazi tofauti uliwafanya watu wawe na asili ya mapato mbalimbali na kupunguza shinikizo la mazingira.[35,36]

→ **Bonyeza Mbele 71**

[MAHOJIANO: Sarah Acieng' Onyango, mwanachama wa jamii ya HoPE-LVB]

"Ujuzi muhimu zaidi nilioupata ni kujenga na kusimamisha stovu za kuhifadhi moto."

"Hii imekuwa sili ziada kwangu ya mapato…"

→ **Bonyeza Mbele 72**

Hope-LVB pia iliwapunguzia jamii migogoro ya watu na wanyama.

→ **Bonyeza Mbele 73**

[MAHOJIANO: Tom Guda, Mwenyekiti, Kitengo cha Usimamizi wa Ufuo wa Afrika Mashariki]

"Kuna migogoro mingi ya watu na wanyama inayotokana na watu kulima sehemu ya milima iliyowachiwa wanyama poli. Hii hufanya sehemu za ufuo wa ziwa kukosa uthabiti na kumomonyoka kwa urahisi katika mfumo wa ekolojia. Tukifanya kazi pamoja na wafanyikazi wa KWS (Kenya Wildlife Service) na pia kufanya kazi kwa pamoja na wenzi wetu kutoka ukulima, jamii ilihisishwa kutolima karibu sana na ufuo wa mito, pia wasilime karibu na ufuo wa ziwa ili kuepuka migogoro."

→ **Bonyeza Mbele 74**

Kwa kupunguza uvuvi wa kupindukia, usalama wa chakula uliangazwa kwa sababu kwa sasa, idadi ya samaki inastawi katika Ziwa Viktoria.[37,38]

→ **Bonyeza Mbele 75**

Kitengo cha Usimamizi wa Ufuo unaoziunga na kushurutisha sheria za uvuvi zilizoimarishwa na jamii kimeshuhudia tofauti kuu katika Ziwa Viktoria.[39,40, 41]

→ **Bonyeza Mbele 76**

[MAHOJIANO: Peter Sikuku, Kitengo cha Usimamizi wa Chuowe]

"Mradi huu ulitusaidia kuteua maeneo ya kufuga samaki kwenye ziwa. Samaki sasa wanazaana na tumepata ongezeko la kutajika la mazao ya samaki."

→ **Bonyeza Mbele 77**

Kutokana na kuvutiwa na matokeo mazuri ya afya na mazingira, maofisa wa kaunti ya Homa Bay waliimarisha idara ya PHE na kamati ya kuiongoza ili kuiratibu juhudi za kikaunti za PHE.[42]

→ **Bonyeza Mbele 78**

Kwa vile ujumbe wa uongozi wa afya na mali ya asili jumuishwa pamoja na mahitaji ya kimsingi ya watu ya kiafya, chakula na riziki zinazoshughulikiwa, jamii nyingi zimeikumbatia mielekeo ya PHE na kuifanya mradi kudumukwa muda mrefu.

→ **Bonyeza Mbele 79**

Mwelekeo wa PHE pia ni ya gharama ya chini inayopunguza mali inayohitajika kutekeleza uongozi wa uzuiaji wa afya na mali asili kwa kujumuisha uratibu inayohusiana na zingine na kuziba ufa unaoachwa na miradi ya sekta moja inayoshughulikia changamoto zingine ambazo jamii hukabiliana nazo.[43]

→ **Bonyeza Mbele 80**

Kutoka 2011-2013, Mpango wa Utafiti wa Kuimarisha Huduma (the Program Research of Strengthening Services) au Mradi wa PROGRESS ikishirikiana na Green Belt Movement, ilionyesha kuwa wafanyikazi wa mazingira wanaweza kuwasilisha habari za afya zifaazo kwa wanajamii zao.[44,45,46]

→ **Bonyeza Mbele 81**

Green Belt Movement iliimarishwa wakati ambapo wanawake walikuwa wanashindwa kushughulikia mahitaji yao ya kinyumbani ya kuni. Shirika hili liliwafunza mtindo wa kupanda miti ya kudumu.[47]

→ **Bonyeza Mbele 82**

Kushughulikia mahitaji ya kiafya ya kijamii, mradi huu wa PROGRESS waliwafunza wataalam wa misitu huko kaunti za Nyeri na Meru njia za kufaa za kueleza ujumbe wa afya ambayo walipitisha inavyofaa kwa jamii yao.[48]

→ **Bonyeza Mbele 83**

Ushirikiano huo ulionyesha kuwa wafanyikazi wasio wa afya wanaweza kupitisha ujumbe inavyofaa na kwa shauku kwa kutoa ujumbe halisi kwa jamii zao.[49]

→ **Bonyeza Mbele 84**

Watu wa hisani wa mradi wa Green pia waliongeza kuwashirikisha wanaume katika mijadala ya upangaji uzazi.[50]

→ **Bonyeza Mbele 85**

Mitazamo iliyojumuisha yanayohusu idadi ya watu, afya na mazingira yanafanyika kote Kenya na ina uwezekano wa kutekelezwa katika sehemu zingine za nchi hii.[51]

→ **Bonyeza Mbele 86**

Miradi hii, pamoja na miradi mingine iliyomo ulimwenguni, inaonyesha kuwa mitazamo ya PHE inafaa na inaongeza thamani mbali na sekta ya idadi ya watu, afya na mazingira kama:

→ **Bonyeza Mbele 87**

Kuwawezesha wanawake pakubwa kiafya na kiuchumi

→ **Bonyeza Mbele 88**

Uelewano na uungaji mkono kwa jamii kwa kuingilia mambo ya kiafya na kimazingira; na

→ **Bonyeza Mbele 89**

Ongezeko la akiba ya wakati na kuhifadhi gharama kwa watekelezaji wa miradi na majumbani.[52]

→ **Bonyeza Mbele 90**

Kwa kuongezea, uwezekano wa miradi ya PHE kuwafikia vijana unaweza kuchangia ukuzaji wa uchumi kwa kasi kwa kujadiliana na kuwawekezea vijana.[53]

→ **Bonyeza Mbele 91**

Mtazamo wa PHE umeonekana kuwa wa kuhifadhi gharama ukilinganishwa na miradi inayoshughulikia sekta moja.54 Wanauchumi wanakadiria kila dola inavyowekezwa katika upangaji uzazi wa hiari na kupunguza matokeo ya ushushaji wa ardhi kwa pauni 4.[55,56] Huku kuhifadhi gharama kwa chini ya PHE katika uwekezaji.

→ **Bonyeza Mbele 92**

Kupunguza ongezeko la idadi ya watu,

→ **Bonyeza Mbele 93**

Kuwekeza kwa afya, na

→ **Bonyeza Mbele 94**

Ulinzi wa mali ya asili ni ya muhimu katika kutimiza ruaza ya Kenya ya 2030 na pia ruaza Maono ya Muungano wa Afrika wa 2063 na Malengo Yanayoendelezwa ya Maendeleo.

→ **Bonyeza Mbele 95**

[MAHOJIANO] Aliyekuwa mbunge, Eneo la Butere, Kaunti ya Kakamega, mheshima Andrew Toboso]

"Serikali ya Kaunti lazima iwe na mpango wao wa maarifa katika utengezaji wa sera zao na waweke rasilmali nyingi kuhakikisha kuwa wametunga sheria ambazo zinahifadhi mazingira, kuona kwamba wanawekeza mali toshelezi katika sekta ya afya kuhakikisha kuwa idadi ya watu walio vijijini wana afya nzuri ya kuwawezesha kuzalisha. Uzalishaji huu utaendeleza uchumi wa kaunti ambao utachangia kuendesha uchumi wa kitaifa."

→ **Bonyeza Mbele 96**

PHE inaweza kuchukua jukumu muhimu katika kuendeleza maendeleo ya uchumi wa kijamii na ubora wa maisha ya jamii mbalimbali.

→ **Bonyeza Mbele 97**

Tunawaomba viongozi wa kitaifa na kaunti kuwa:

Kuthibitisha msimamo wao kwa PHE kama utekelezaji wa maendeleo…

→ **Bonyeza Mbele 98**

…kuzichunguza sera zilizomo ili kuiongoza na kuikuza mielekeo ya walio wengi wa PHE katika sekta tofauti,

→ **Bonyeza Mbele 99**

na kutafsiri sera ili PHE iitekeleze ifaavyo.

→ **Bonyeza Mbele 100**

Kenya inaweza kutafuta ushauri kutokana na maarifa ya PHE uliokuzwa na Jamii ya Afrika Mashariki (East African Community).

→ **Bonyeza Mbele 101**

Serikali ya Kitaifa inafaa kuunda kizingiti cha kazi cha sheria kuisaidia mielekeo ya watu wengi katika PHE…

→ **Bonyeza Mbele 102**

…na kukuza uwezekano wa wakala za serikali kutekeleza mitazamo ya PHE ifaavyo.

→ **Bonyeza Mbele 103**

Serikali za kaunti zinafaa kuimarisha utaratibu wa asasi kusimamia sekta zote, kujumuisha PHE kwa mipango ya maendeleo ya kaunti…

→ **Bonyeza Mbele 104**

…kuimarisha ahadi zao za kifedha na kutenga rasilmali kwa PHE.

→ **Bonyeza Mbele 105**

Mashirika ya kiraia yanayofanya kazi katika sekta tofauti yanafaa kutafuta nafasi ya kushirikiana na juhudi za PHE na wauunge mkono utengenezaji wa rasilmali katika kiwango cha kitaifa na kaunti.

→ **Bonyeza Mbele 106**

[MAHOJIANO: Mchungaji John Akuno, Kaunti ya Kisumu]

"Kutokana na faida tuliyoiona hapa, kama inaweza kuendelezwa kwa jamii zingine, inaeza kusaidia sana. Inaweza kuwasaidia watu wengi kujua wanavyoweza kudhibiti idadi ya watu wao, kujua kudhibiti huduma za afya na kuhifadhi mazingira yao."

→ **Bonyeza Mbele 107**

Ni wakati unaofaa kwa Kenya kuchukua uongozi kwa maendeleo inayotekelezeka kwa kushughulikia athari zote za huduma za afya kutopatikana kwa urahisi, nafasi pungufu za uchumaji wa mapato, udidimishaji wa mali ya asili na athari za hali ya anga.

→ **Bonyeza Mbele 108**

Kila mtu ana jukumu lake la kufanya lakini la muhimu zaidi ni viongozi wa kitaifa na kaunti lazima waudhihirishe msimamo wa ustawi wa Wakenya kuimarisha siku za mbeleni za nchi yetu kwa kuwekeza katika mitindo ya ujumuishaji wa PHE.

→ **Bonyeza Mbele 109**

Kwa kutambua uhusiano ulioko kati ya watu wa Kenya, afya zao na utekelezaji wa mali ya asili na tukiyashughulikia sasa, tunaweza kuiweka Kenya katika njia ya kufaulu kiuchumi na malengo yao ya kimaendeleo na kuendeleza ubora wa maisha ya mamilioni ya Wakenya huku wakihifadhi mazingira yetu kwa vizazi vya siku za usoni.

# MAREJELEO


1 Serikali ya Jamhuri ya Kenya, *Kenya Vision 2030, The Popular Version* (Nairobi: Government of the Republic of Kenya).
2 United Nations, "Sustainable Development Goals," (2016), inayopatikana kwa www.un.org/sustainabledevelopment/sustainable-development-goals/.
3 National Council for Population and Development (NCPD), Ministry of State for Planning, National Development and Vision 2030, *Sessional Paper No. 3 of 2012 on Population Policy for National Development* (Nairobi: NCPD,2012).
4 Serikali ya Jamhuri ya Kenya, Wizara ya Mazingira na Madini, *National Climate Change Action Plan 2013-2017: Executive Summary* (Nairobi: Serikali ya Jamuri ya Kenya, 2010).
5 United Nations, (UN) Population Division, *World Urbanization Prospects: The 2014 Revision* (New York: UN, 2013).
6 Kristen P. Patterson na Smita Gaith, "Population Health and Environment," Global Health e-Learning Center, inayopatikana kwa www.globalhealthlearning.org/course/population-health-and-environment.
7 Kenya National Bureau of Statistics, Wizara ya Afya/Kenya, National AIDS Control Council/Kenya, Kenya Medical Research Institute, NCPD, na ICF, Kenya Demographic and Health Survey (DHS) 2014 (Rockville, MD: ICF).
8 KNBS, Ministry of State for Planning, National Development and Vision 2030, "2009 Kenya Populaton and Housing Census, Analytical Report on Population Dynamics: (2012), inayopatikana kwa www.knbs.or.ke/publications/.
9 KNBS, "Population and Housing Census 2009" (2012).
10 Kenya National Bureau of Statistics (KNBS), Economic Survey2017, (Nairobi: KNBS, 2017).
11 Feed the Future, "Kenya Fact Sheet," inayopatikana kwa https://feedthefuture.gov/sites/default/files/resource/files/ftf factsheet kenya jan2013.pdf.
12 KNBS, Economic Survey 2017.
13 Population Reference Bureau(PRB), *Kenya Population Data Sheet 2011* (Washington, DC: PRB, 2011).
14 United States Agency for International Development (USAID) Land and Urban Office, "Kenya," (Februari 2017), inayopatikana kwa www.land-links.org/country-profile/kenya/.
15 KNBS, Economic Survey 2017.
16 Rachel Winnik Yavinsky et al.,"The Impact of Population, Health and Environment Projects: A Synthesis of Evidence," (2015), working paper, inayopatikana kwa http://evidenceproject.popcouncil.org/wp-contents/uploads/2015/06/PHE-Synthesis-Report1.pdf.
17 Lattice Consulting, "Market Study Of The Aquaculture Market in Kenya: Kenya Market-Led Aquaculture Program (KMAP)," (Juni 2016), inayopatikana kwa www.farmafrica.org/downloads. study-of-the-kenyan-aquaculture-market.pdf.
18 Jesse T. Njoka et al., "Kenya: Country Situation Assessment," (Januari 2016), working paper, inayopatikana kwa http://prise.odi.org/wp-content/uploads/2016/01/Low-Res Kenya-CSA.pdf.
19 UN Environment Program (UNEP), Convention on Biodiversity, "Kenya-Country Profile," (2017), inayopatikana kwa https://www.cbd.int/countries/profile/default.shtml?country=ke.
20 UNEP, *Kenya: Atlas of Our Changing Environment* (Nairobi: UNEP,2009)
21 Jesse T. Njoka et al., "Kenya: Country Situation Assessment,"
22 AFIDEP and PAI, "Population, Climate Change and Sustainable Development in Kenya, "(2012), inayopatikana kwa https://pai.org/wp-content/uploads/2013/01/Kenya PIB F inal.pdf.
23 UNEP, *Kenya.*
24 Sam Sellers, *Gender and Climate Change: A Closer Look at Existing Evidence, 2016,* inayopatikana kwa http://wedo.org/gender-and-climate-change-a-closer-look-at-existing-evidence-ggca/.
25 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
26 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
27 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
28 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Victoria Basin, Technical rief," (Juni 2015), inayopatikana kwa www.pathfinder.org/wp-content/uploads/2016/09/Sustaining Rights 2015PHE.pdf.
29 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
30 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
31 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
32 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
33 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
34 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
35 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
36 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
37 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
38 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
39 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
40 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
41 Pathfinder International, "Bringing Fishing and Planning for Families Together in the Basin," (2016), inayopatikana kwa www.pathfinder.org/wp-content/uploads/2016/06/HoPE-LVB-Beach-Management-Units.pdf.
42 Pathfinder International, "Sustaining Health, Rights and the Environment in the Lake Basin."
43 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
44 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
45 Agatha Mbulo na Nancy Waceke," Green Belt Movement (GBM)'s Environment Health and Population Project, (2013), inayopatikana kwa www.greenbeltmovement.org/node/421.
46 FHI 360, "Linking Population, Environment and Health: The GBM Experience," (2013), inayopatikana kwa www.youtube.com/watch?v=BSOauSpM ew.
47 Lisa Merton na Alan Dater, "Taking Root: The Vision of Wangari Maathai," inayopatikana kwa www.greenbelt movement.org/wangari-maathai/taking-root-documentary.
48 FHI 360, "Linking Population, Environment and Health."
49 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
50 Mbulo na Waceke, "GMB's Environment Health and Population Project."
51 PRB, "Population, Health and Environment (PHE) Activity Map" (2016), inayopatikana kwa www.prb.org/About/ProgramsProjects/PHE/PHE-activity-map.aspx.
52 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
53 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
54 Yavinsky et al., "The Impact of Population, Health and Enviroment Projects."
55 National Council for Population and Development (NCPD, "Family Planning in Kenya: Saving Lives, Saving Money" (2015), inayopatikana kwa https://www.healthpolicyproject.com/486 KenyaimpactNowOnepager.pdf
56 Ephraim Nkonya, Alisher Mirzabaev na Joachim von Braun, ed., *Economics of Land Degradation and Improvement – A Global Assessment for Sustainable Development* (New York: Springer International, 2016).

# Ujumbe Maalum Kutoka Kwa Maandishi



Kenya ni kiongozi humu Afrika sanasana katika sera za maendeleo na mipango ya kuimarisha uchumi,kijamii na ustawi wa kisiasa wa watu na kuimarisha uchumi.[1]

Hata hivyo, mengi bado yanafaa kushughulikiwa kujumuisha idadi ya watu inayokua kwa haraka, afya na ustawi wetu na tunavyotumia rasilmali yetu.

Kenya inaweza kuwa kiongozi katika kuendeleza afya,utekelezaji wa mazingira na ustawi zaidi wa uchumi kwa kushughulikia changamoto zote tatu pamoja.




Mtazamo wa Idadi ya watu, Afya and Mazingira, au PHE,inatambua uwiano tata wa watu, afya zao na rasilmali wanayotegemea.

PHE inajumuisha habari za upangaji uzazi kwa hiari na huduma za kimsingi za kutunza afyana udhibiti wa mali ya asili inayotekelezeka.



Katika jamii za vijijini – ambapo robo tatu ya Wakenya wanapoishi na ambapo miradi mingi ya PHE yaliyojumuishwa - afya na riziki zinahusiana na udhibiti wa mali ya asili na usalama wa chakula.[2]

Muundo msingi wa usafiri na afya nyonge – sanasana katika sehemu za mbali – zinawazuia familia kupata huduma za afya, hata afya ya uzazi.




Katika jamii za Kenya vijijini na walio maskini, wanawake mara nyingi huwazaa watoto wawili zaidi ya walivyotarajia. Kutokana na hayo, familia huhitaji rasilmali zaidi ili kuwakimu wote, hali hii yaweza kuongeza umaskini kinyumbani na kitaifa.[3]

Familia inapokuwa na watoto wengi kuliko walivyotarajia, idadi ya watu pia hukua haraka. Idadi ya watu Kenya iliongezeka marudufu kutoka milioni 21 mwaka wa 1989 hadi milioni 44 mwaka wa 2015 na inasemekana kuwa itafika milioni 64 ikifika 2030.[4]



Ongezeko la idadi ya watukwa haraka unaweza kuathiri mazingira na vile watu wanatumia mali yao ya asili.

Misitu inakatwa kwa kiwango cha kuogofya ili kupambana na mahitaji ya ardhi ya kulima, machungani, kuni na makazi na maziwa yanadidimia katika uvuvi wa samaki kutokana na mitindo ya uvuvi isiyotekelezeka na mipango ya viwanda.[5]




Kwa kuongezea, mabadiliko ya hali ya anga na matukio ya hali ya anga yaliyozidi kama ukame yanaharibu mimea na mifugo ambayo hutanguliza ukosefu wa usalama wa chakula, upungufu wa mapato kwa familia na umaskini uliokithiri.[6]

